ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE PANDU AMEIR KIFICHO

1. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	Kuteuliwa na Rais
2. Mhe. Omar Othman Makungu	Mwanasheria Mkuu
3.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
4.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
5.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
6.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	Jimbo la Magogoni
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Jimbo la Mgogoni
8.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	Jimbo la Donge
10.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
11.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
12.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
13.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
14.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
16.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
17.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake
18.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
19.Mhe. Farida Amour Moh'd	Nafasi za Wanawake
20.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Kuteuliwa na Rais
21.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
22.Mhe. Haji Faki Shaali	imbo la Mkanyageni
23.Mhe. Haji Mwadini Makame	Jimbo la Nungwi
24.Mhe. Haji Omar Kheri	Jimbo la Tumbatu
25.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
26.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
27.Mhe. Haroun Ali Suleiman	Jimbo la Makunduchi
28.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
29.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
30.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
31.Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Jimbo la Chwaka
32.Mhe. Jaku Hashim Ayub	Jimbo la Muyuni
33.Mhe. Juma Duni Haji	uteuliwa na Rais
34.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
35.Mhe. Machano Othman Said	Jimbo la Chumbuni
36.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
37.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
38.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
39Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
40.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake

41.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
42.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
43.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
44.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	Kuteuliwa na Rais
45.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
46.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
47.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
45.Mhe. Mussa Khamis Silima	Jimbo la Uzini
46.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
47.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	Jimbo la Dimani
49.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Jimbo la Mtoni
50.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
51.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
53.Mhe. Omar Yussuf Mzee	Kuteuliwa na Rais
54.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
55.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
57.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
59.Mhe. Said Ali Mbarouk	Jimbo la Gando
60.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
61.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
62.Mhe. Salma Moh'd Ali	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
65.Mhe. Salum Amour Mtondoo	Jimbo la Bububu
67.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	imbo la Mwanakwerekwe
69.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
70.Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya	Kuteuliwa na Rais
71.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
72.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
73.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	Jimbo la Jang'ombe
74.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Jimbo la Fuoni
75.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
76.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
77.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
78.Mhe. Zahra Ali Hamad	Nafasi za Wanawake
79.Mhe. Zainab Omar Mohammed	Kuteuliwa na Rais

BARAZA LA NANE LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KWANZA

Kikao cha Kwanza – Tarehe 9 Novemba, 2010

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

WIMBO WA TAIFA WA ZANZIBAR

Katibu wa Baraza la Wawakilishi: Kwa kunukuu kanuni ya 21, Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2009 kama ifuatavyo:

Kanuni ya 21:

> "Bila ya kuathiri masharti ya katiba Mkutano wa Kwanza wa Baraza jipya utaanza tarehe ile ambayo Baraza jipya limeitishwa na rais kukutana."

Vile vile kanuni ya 22 (2) inaelekeza kama ifuatavyo:

> "Mwanzoni mwa kikao cha kwanza cha Mkutano wa Kwanza wa Baraza jipya Katibu atasoma tangazo la rais la kuliita Baraza jipya kukutana kisha atasoma dua."

Waheshimiwa Wajumbe kwa heshima kubwa sasa naomba nilisome tangazo la rais la kuliita Baraza jipya kukutana.

Hati ya kuitisha Mkutano wa Baraza la Wawakilishi chini ya kifungu cha 91 (1) cha Katiba.

"Mimi Dk. Ali Moh'd Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uwezo niliopewa chini ya kifungu cha 91 (1) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984, naamuru kwamba Mkutano wa Baraza la Wawakilishi ufanyike kwa ajili ya kuendelea na shughuli zake kuanzia tarehe 9 Novemba, 2010 saa 3:00 asubuhi."

Imetiwa saini na muhuri wa serikali tarehe 4 Novemba, 2010 na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Moh'd Shein.

DUA

Katibu (Ibrahim Mzee Ibrahim) alisoma dua

UCHAGUZI WA MHE. SPIKA

Katibu: Waheshimiwa Wajumbe hatua ya kwanza kabisa ni uchaguzi wa Spika kwa sababu maelekezo ya vifungu vya katiba yanasema "Hakuna shughuli yoyote ya Baraza itakayoendelea wakati kiti cha Uspika kiko wazi." Kwa hivyo, ajenda ya kwanza kabisa ni uchaguzi wa Spika.

Katibu: Waheshimiwa Wajumbe sanduku la kupigia kura halina kitu na tunali-*lock* sasa hivi kwa *seal* maalum.

Wasaidizi wetu wanagawa karatasi za kupigia kura na kama tunavyoelewa wagombea ni wawili, mgombea kutoka Chama cha CUF Mhe. Abass Juma Muhunzi na mgombea kutoka Chama cha Mapinduzi Mhe. Pandu Ameir Kificho. Kwa hivyo, tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe uweke *tick* katika mgombea ambaye unapenda awe Spika wa Baraza la Wawakilishi.

Utaratibu wa shughuli zetu za Baraza kwa kweli hatuna *tradition* ya wagombea kujieleza. Wagombea nyote mnawafahamu kwa hivyo tunakwenda moja kwa moja kwenye kupiga kura.

Naomba tuhakikishe kwamba kila Mhe. Mjumbe amepata *ballot paper*. Nadhani kila Mhe. Mjumbe tayari amepata karatasi ya kupigia kura. Kuna mheshimiwa yeyote ambaye hajapata karatasi ya kupigia kura, hakuna. Kwa hivyo, tayari tumepiga kura zetu. Haya tuanze zoezi la kukusanya kura.

Waheshimiwa Wajumbe tumemaliza zoezi la kupiga kura na kwa taarifa niliyoipata Mhe. Abass Juma Muhunzi amesema kwamba anamteua Mhe. Salim Abdalla Hamad wa Jimbo la Mtambwe kuwa wakala wake katika kuhesabu na Mhe. Pandu Ameir Kificho yeye amemteua Mhe. Machano Othman Said kuwa wakala wake katika zoezi la kuhesabu kura. Kwa hivyo, waheshimiwa tuliowataja tutakapotoka kwenda katika zoezi la kuhesabu kura tunawakaribisha katika *Committee Room No. 2*. Kila wakala mmoja kwa kila mgombea tutakuwepo hapo na tutaahirisha Baraza kwa muda wa nusu saa ili kujipa muda wa kuhesabu hizo kura na kuja kutoa matokeo. Kwa hivyo, naomba kuahirisha Baraza kwa muda wa nusu saa.

(Saa 3:15 asubuhi Baraza liliahirishwa kwa muda wa nusu saa kwa ajili ya kwenda kuhesabu kura)

(Saa 3:45 asubuhi Baraza lilirudia)

MATOKEO YA UCHAGUZI WA SPIKA

Katibu: Waheshimiwa Wajumbe sasa naomba nitangaze matokeo ya uchaguzi wa Spika uliofanyika muda mfupi uliopita leo tarehe 9 Novemba, 2010. Idadi ya kura zilizopigwa zilikuwa ni kura 78, kura zilizoharibika ni kura moja. Idadi ya kura alizopata Mhe. Abass Juma Muhunzi ni kura 32 na idadi ya kura alizopata Mhe. Pandu Ameir Kificho ni kura 45.

Kutokana na matokeo hayo sasa ninamtangaza rasmi Mhe. Pandu Ameir Kificho kwamba amechaguliwa kuwa Spika wa Baraza hili la Nane la Wawakilishi la Zanzibar kwa kipindi cha 2010 hadi 2015. *(Makofi)*

Kwa kuwa wagombea wote wawili walikuwa na wasi wasi mkubwa waliamua kujificha sehemu. Sasa labda niwaombe Mhe. Machano Othman Said ambaye alikuwa ni wakala wa Mhe. Pandu Ameir Kificho na pia Mhe. Salim Abdalla Hamad ambaye alikuwa ni wakala wa Mhe. Abass Juma Muhunzi. Lakini pia tupate *flavor* ya waheshimiwa wanawake.

Kwa hivyo, namtaka Mhe. Amina Iddi Mabrouk kwa upande wa CCM na Mhe. Zahra Ali Hamad kwa upande wa CUF wakamtafute mgombea. Tunaomba mkamlete mgombea aliyechukua nafasi ya pili, lakini pia na mshindi Mhe. Pandu Ameir Kificho. Tafadhalini sana.

KIAPO CHA MHE. SPIKA

Katibu: Mhe. Pandu Ameir Kificho ninayo heshima kukuarifu kwamba Wajumbe wa Baraza hili tukufu katika kutekeleza Katiba ya Zanzibar na katika kutumia haki na fursa walizopewa kwa mujibu wa sheria wamekuchagua wewe uwe Spika wa Baraza hili. Kutokana na kuchaguliwa kwako huko sasa nakuita wewe Mhe. Pandu Ameir Kificho uape kiapo cha uaminifu kisha ukalie kiti cha Baraza hili ukiwa Spika. Karibu sana Mhe. Spika.

(Hapa Mhe. Spika aliapishwa na kukalia kiti chake)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujumuisha hapa katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi tukiwa sote ni wajumbe wapya. Tumezaliwa baadhi yetu baada ya mchakato wa tarehe 31 mwezi uliopita na mimi nimezaliwa leo. Kwa hiyo, nyote nyinyi ni wapevu zaidi kuliko mimi.

Lakini pili nichukue nafasi hii pia kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuupitisha uchaguzi wetu salama usalmini pale tarehe 31 Oktoba, mwaka huu na leo hii afisi ya Baraza ikapanga kwamba kazi ya kwanza iwe ni kumchagua Spika, ili baadae tena tuweze kufanya shughuli nyengine za kuwaapisha wajumbe wenzangu.

Nichukue nafasi hii kusema kwamba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi mlikaa, mkachekecha na hatimae mkapiga kura ambao pia uchaguzi huu kwa jinsi mlivyotulia na jinsi vile ambavyo wapambe walikuja kunichukua kule ambako nilijificha nilikuwa mbali kweli. Walipokuja nikawauliza hivi mnanipeleka wapi? Wakanambia twendezetu kuna kazi kule ukatusaidie. Nikawaambia kwanza nimtafute mgombea mwenzangu Mhe. Abass Juma Muhunzi, naomba nimtambulishe nafikiri yupo, eee yule pale.

Mhe. Abass Juma Muhunzi alipokuja tukazungumza kunong'ona ilinimaanisha kwamba uchaguzi huu ulikuwa huru na haki. Wale wapambe wa pande zote mbili walipokuja wakatuchukua sote kwa pamoja nikaamini na nikapata faraja na moyo kwamba uchaguzi umekwenda vizuri sana. Hivyo, nichukue nafasi hii Waheshimiwa Wajumbe kukushukuruni sana kwa kuendesha uchaguzi mzuri, huru na haki kiasi cha kwamba naingia hapa nimepata moyo mkubwa sana wa kufanya kazi na nyinyi Waheshimiwa Wajumbe, baada ya kuona mnanikaribisha kwa makofi mengi kuonesha kwamba nyote mmefurahika juu ya namna uchaguzi ulivyokwenda.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni sana kwa kazi nzuri mliyoifanya na sasa niko tayari kuweza kushirikiana nanyi katika kazi ya pili ambayo Katibu ananieleza ni ya kuwaapisha nyinyi wajumbe wenzangu.

Kabla ya kufanya hivyo, naomba niwakaribishe wageni wetu wote wakiwemo mabalozi wa sehemu mbali mbali, pamoja na balozi wetu Washington kutoka Afrika Mama Amina Salum Ali, yule pale. *(Makofi)*

Kwa kuwa sina orodha ya wale wageni wetu waliofika hapa, isipokuwa yeye alipoingia tumeingia sambamba nilijua kwamba yupo katika shughuli yetu hii ya uchaguzi wa Spika na vile vile kuwaapisha Waheshimiwa Wajumbe.

Kwahiyo nakukaribisheni nyote wageni wetu mliohudhuria hapa ili mshuhudie kazi yetu leo ya kwanza ambayo moja mmeshaishuhudia lakini ya pili ni kuwaapisha waheshimiwa wajumbe. Waheshimiwa wageni wetu karibuni sana.

KIAPO CHA UAMINIFU

Wajumbe wafuatao waliapa kiapo cha uaminifu na kukaa katika nafasi zao.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla - Jimbo la Chonga

Mhe. Spika: Mhe. Abdalla Juma Abdalla anapewa zana nono za kufanyia kazi, ambayo ni Katiba mbili nayo ni Katiba ya Zanzibar na Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania pamoja na Kanuni ya Baraza. Karibu sana Mheshimiwa Abdallah.

Mhe. Abdalla Moh'd Ali - Jimbo la Mkoani.
Mhe. Abdi Mosi Kombo - Jimbo la Matemwe

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe, wakati Mheshimiwa anachukua nafasi yake, nimeshauriwa kwamba Mjumbe huenda akitoka kutoka kwenye kiti chake mpaka hapa ni mbali sana anaweza akafika hapa *pressure* kidogo imepanda juu. Nafikiri orodha hizi kila mjumbe anayo, kuna kiti kimoja hapa mbele kitupu, baada ya yule anaekuja hapa, yule anayefuatia tumuombe akae hapa ili apoe kidogo halafu akimaliza yule itakuwa anaingia bila ya kuwa na *pressure* ya aina yoyote. Wahudumu watasaidia utaratibu huu ili tuone kwamba tunamaliza kazi hii kwa muda mfupi.

Mhe. Abdillah Jihad Hassan	Jimbo la Magogoni
Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Jimbo la Mgogoni
Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
Mhe. Ali Juma Shamuhuna	Jimbo la Donge
Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

Mhe. Spika: Huyu ni mmoja kati ya wapambe waliokuwa wamenileta humu ukumbini baada ya kura za uchaguzi wa Spika kuhesabiwa, baada ya kumuona yeye sikupata tabu nikaja.

Mhe. Asaa Othman Hamad Jimbo la Wete

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabda hatujaendelea naomba ridhaa yenu, kuna mpiga picha mmoja ambaye kwenye sherehe nyingi sana huwa anapiga picha. Ameniomba na mimi nikamjibu kwamba nitaomba ridhaa kwa wajumbe, ili aingie kwa karibu na yeye aweze kuchukua picha. Hapana shaka mnamjua anaitwa Zahor Ramj. Naomba ridhaa yenu mkubali kama wenzake ili na yeye aingie kuja kuchukua picha ambayo itakuwa ni kumbukumbu nzuri.

Namuomba ndugu Zahor Ramj aingie ili na yeye achukue picha za shughuli hii ya uapishaji. Lakini kwa kuwa nafasi zetu ndogo nadhani nitakuwa sikufanya haki vizuri kusema kwamba kuna wengine wengi wanaweza kutaka, lakini nafasi yetu ni ndogo sana. Huyu kwa ombi maalum na kwa ridhaa yenu nakushukuruni sana aingie kuchukua picha.

Ndugu Zahor karibu.

Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake
Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
Mhe. Farida Amour Moh'd	Nafasi za Wanawake
Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Kuteuliwa na Rais
Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
Mhe. Haji Faki Shaali	Jimbo la Mkanyageni
Mhe. Haji Mwadini Makame	Jimbo la Nungwi
Mhe. Haji Omar Kheri	Jimbo la Tumbatu
Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
Mhe. Haroun Ali Suleiman	Jimbo la Makunduchi
Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Jimbo la Chwaka
Mhe. Jaku Hashim Ayub	Jimbo la Muyuni
Mhe. Juma Duni Haji	Kuteuliwa na Rais
Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
Mhe. Machano Othman Said	Jimbo la Chumbuni
Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	Kuteuliwa na Rais
Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
Mhe. Mussa Khamis Silima	Jimbo la Uzini
Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	Jimbo la Dimani
Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Jimbo la Mtoni
Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
Mhe. Omar Othman Makungu	Mwanasheria Mkuu
Mhe. Omar Yussuf Mzee	Kuteuliwa na Rais
Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	Kuteuliwa na Rais
Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
Mhe. Said Ali Mbarouk	Jimbo la Gando
Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
Mhe. Salma Moh'd Ali	Nafasi za Wanawake
Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
Mhe. Salum Amour Mtondoo	Jimbo la Bububu
Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	Kuteuliwa na Rais
Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya	Kuteuliwa na Rais
Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
Mhe. Suleiman Othman Nyanga	Jimbo la Jang'ombe
Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Jimbo la Fuoni
Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Mhe. Zahra Ali Hamad	Nafasi za Wanawake
Mhe. Zainab Omar Mohammed	Kuteuliwa na Rais

Katibu: Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli ya kiapo cha uaminifu kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi imekamilika na pia napenda kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizopangwa kutekelezwa kwa siku hii ya leo hivi sasa zimekamilika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nichukuwe nafasi hii tena kuwashukuru wajumbe wote kwamba sasa mko tayari kwa kazi baada ya kula kiapo cha uaminifu. Waheshimiwa Wajumbe, kama tunavyojua kwamba leo katika

shughuli zetu tumefanya kazi mbili kubwa ambayo ni kumchagua Spika, na akaapishwa na hatimaye kuwaapisha Waheshimiwa Wajumbe.

Mtakumbuka kwamba katika Baraza lililopita la saba kwenye shughuli moja muhimu sana iliyofanywa na Baraza ambalo baadhi ya wajumbe humo ndani ilikuwa ni kupitisha mswada wa kura ya maoni, mswada ambao nia na madhumuni yake ilikuwa kuipa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar mamlaka ya kuandaa suala zima la kura ya maoni yaani *referendum*.

Mkutano huo ulikuwa ni mkutano muhimu sana na ulisababisha tuweze kurekebisha katiba. Tulifanya hivyo, kwa hivyo katiba mliyopewa ni katiba iliyojumuisha marekebisho tuliyofanya kwenye Baraza hilo la Saba, mnamo mwezi wa Agosti. Kura ya maoni ilifanyika na wananchi walielekeza kwamba nchi yetu iende kwa mfumo wa serikali ya Umoja wa Kitaifa. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe tuelewe kwamba Baraza hili moja kati ya kazi yake muhimu kama vile tulivyoapa hapa, kwamba tutatetea na kulinda katiba ya Zanzibar na katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, basi katika kuapa huko umeapa kwamba utailinda na kuitetea Serikali ya Umoja wa Kitaifa, kwa sababu suala hilo limo ndani humu.

Kwa hivyo, tuelewe moja kati ya kazi yetu kubwa baada ya maelekezo ya wananchi, pale tarehe 31/07/2010 waliporidhia suala zima la Serikali ya Umoja wa Kitaifa, kwa hivyo wajumbe sisi tuliomo humu ndani, tunapaswa na ni wajibu wetu kulinda mfumo huo mpya wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, kwa sababu ndio ulioridhiwa na wananchi, lakini pia ndio ambao Baraza la Saba lililopita baadhi ya wajumbe tukiwemo humu tulipitisha katiba kwa kufanya marekebisho na kuuingiza utaratibu huo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Kwa hivyo, nakuombeni Waheshimiwa Wajumbe tuelewe kwamba hiyo ndio azma ya wananchi pamoja na Baraza. Kwa hivyo, huo ndio wajibu wetu sote kwa mashirikiano kulinda Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Kwa kweli, hilo nilitaka niliseme kwa lengo la kuwakumbusha Waheshimiwa Wajumbe wajibu wetu.

Suala jengine ni kwamba bado Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi hajateua serikali hiyo. Kwa hivyo, ukaaji wetu leo humu tumekuwa huru kukaa pahala popote. Kwa kawaida na ndio utaratibu unaoeleweka ambao ni uzoefu wetu, kwamba huu mstari wa mbele wanakaa wajumbe wa serikali, ambapo bado hatuwajui nani na nani.

Kutokana na hali hiyo, inaweza kutokea marekebisho kidogo ya namna ya ukaaji, kwamba huu mstari wa mbele na pengine na nyuma kwa kiasi fulani

kwa kadri ukubwa wa serikali utakavyokuwa, basi tutawaomba Waheshimiwa Wajumbe wawapishe mawaziri wetu ambao watateuliwa.

Waheshimiwa Wajumbe, tukio hili tulilolifanya leo lina umuhimu mkubwa na Mhe. Rais wa Zanzibar hapana shaka alikuwa akisubiri tufanyekazi hii, baada ya hapo aweze kuteua hao mawaziri, kwa sababu mawaziri wanatokana na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Kwa hivyo, wajumbe mliopo hapa baadhi yenu mtadiriki kuupata uwaziri. Kwa maana hiyo, natanguliza shukurani na pongezi kwa wale ambao wataupata uwaziri huo.

Vile vile najaribu kwenda hivi msijemkasema umemtizama fulani labda yeye ndiye, aa! Hapana. Kwa hiyo, natembeza macho yangu huku na kule kwa kuepusha kuyaweka kwa mtu mmoja na kuonekana labda waziri wenyewe ndiye huyo Mhe. Hamad Masoud Hamad, huo ni mfano. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa kweli leo tumefanyakazi moja kubwa muhimu, ambayo itampa nafasi pamoja na fursa Mhe. Rais kuunda Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuwateua mawaziri pengine na manaibu mawaziri. Hilo ni jambo la pili.

Pamoja na hayo, kama tulivyoelezwa kwamba leo shughuli yetu kubwa katika Orodha yetu ya Shughuli za Leo na nilivyotangulia kusema, ilikuwa ni kuchagua Spika na hatimaye kuwaapisha wajumbe. Kazi hiyo tayari imeshamalizika.

Pia kama alivyotoa taarifa Katibu wa Baraza la Wawakilishi, kwamba jioni leo hakutakuwa na shughuli yoyote. Lakini nimeombwa niwakumbushe kwamba kesho kutakuwa na semina pale *Ocean View Hotel*. Semina ambayo madhumuni yake makubwa ni kuwapa uelewa Waheshimiwa Wajumbe wote juu ya mambo yetu yanayohusu Baraza, Kanuni pamoja na mengineyo.

Kwa hivyo, nitaomba sana semina hiyo tuhudhurie kesho tarehe 10 Novemba, 2010 pale *Ocean View Hotel* saa 3:00 za asubuhi tuwe tayari tumeshakaa, bila ya shaka *registration* zitaanza mapema kabla ya hapo na semina hiyo inategemewa kuanza saa 3:00 za asubuhi.

Waheshimiwa Wajumbe nyote nakuombeni tuhudhurie semina hiyo, kwa ajili ya kupata uelewa wa shughuli zetu pamoja na mwenendo wetu wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Suala la jengine, naomba kuchukua nafasi hii Waheshimiwa Wajumbe kukupongezeni tena. Nadhani ni vyema nitangulie kuwapongeza wananchi kwa

kukamilisha zoezi la uchaguzi vizuri kwa utulivu na usalama na hatimaye kuchaguliwa nyinyi kutoka majimboni. Vile vile kutokana na uchaguzi huo ndio wakapatikana Wajumbe wa Viti Maalum, ambayo kazi hiyo imefanywa kwa busara na hekima na utulivu mkubwa na Tume yetu ya Uchaguzi wa Zanzibar.

Naomba niwapongeze nyinyi Waheshimiwa Wajumbe mliochaguliwa na wale wa Viti Maalum, pamoja na hayo niwapongeze wale walioteuliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar akiwemo Mwanasheria Mkuu, ambaye aliteuliwa juzi tu na kuapishwa jana, kwa sababu hiyo naye amekuwa mjumbe wetu ndio maana tumemuapisha hapa.

Kwa hivyo, naomba kuchukua nafasi hii kuwapongeza wote pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa kukamilisha zoezi hili la uchaguzi na hatimaye leo hii kuapishwa katika ukumbi wetu.

Pia nichukue nafasi kwa kutoa shukurani maalum kwa Tume yetu ya Uchaguzi ya Zanzibar, ambayo wao kwa kazi nzuri waliyofanya ndio hatimaye leo tumekutana hapa na kufanyakazi ambayo tumetakiwa kuifanya.

Hivyo ni vyema kuwashukuru nyote kwa mara nyengine tena kwa kuamua mimi niwe mtumishi wenu. Kwa hiyo, nataka niahidi mbele yenu hapa kwamba nitafanya jitihada kubwa ya ziada, ili niweze kuwatumikia vizuri Waheshimiwa Wajumbe wote mliopata nafasi na kubahatika kuwa Wajumbe wa Baraza hili la Nane la Wawakilishi. Nakushukuruni sana. *(Makofi)*

Vile vile naomba nimshukuru sana ndugu yangu na kijana wangu Katibu wa Baraza la Wawakilishi pamoja na wafanyakazi wenzake wote kwa kufanyakazi nzuri na matayarisho mazuri, hatimaye kuweza kufanya uchaguzi hapa asubuhi. Kwa kweli mara baada ya kuapishwa kila mjumbe akapata zana za kufanyiakazi, ambazo ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Katiba ya Zanzibar na Kanuni za Baraza la Wawakilishi.

Hizo ndizo zana ambazo tunatakiwa tufanyiekazi kwa kipindi chote cha miaka mitano kuanzia leo hii, bila ya kuacha na kuwasahau wajumbe au wananchi wetu waliotuchagua na kutuleta humu, kwa sababu hao ndio sababu ya kuwemo humu.

Kwa hiyo, ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim Katibu wa Baraza la Wawakilishi nakupongeza sana pamoja na wafanyakazi wote kwa kazi nzuri mlioifanya. *(Makofi)*

Mwisho nataka nichukue nafasi hii kukuelezeni na tutawakumbusha tena baadaye siku ya tarehe 11 Novemba, 2010 tunategemea Baraza letu hili la Nane lihutubiwe na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein saa 4:00 za asubuhi.

Mhe. Rais ameshakubali hivyo na tayari ametuletea taarifa ya ujio wake. Taarifa hiyo, nitakuja kuisoma rasmi siku ya tarehe 11 Novemba, 2010 mapema saa 3:00 asubuhi kabla ya kuja kwake pamoja na ratiba ambayo itafuatana na shughuli hizo.

Waheshimiwa Wajumbe, mpaka hapa kwa leo tumemaliza shughuli zetu na ninaomba nichukue nafasi hii tusimamishe shughuli zetu hadi siku ya tarehe 11 Novemba, 2010 saa 3:00 asubuhi.

(Saa 6:05 mchana kikao kiliahirishwa hadi
tarehe 11/11/2010 saa 3:00 asubuhi)